

Ukweli Kuhusu Chanjo za COVID-19

Ili kukomesha janga hili, tunahitaji kutumia njia zote za kuzuia. Chanjo ni moja wapo ya njia bora zaidi ya kulinda afya yako na kuzuia ugonjwa huu. Chanjo hufanya kazi na kinga asili ya mwili wako ili mwili wako uwe tayari kupambana na virusi ikiwa utaambukizwa. Hatua zingine kama kuvaa mask ama barakoa inayofunika pua na mdomo na kukaa angalau futi sita ama mita mbili kutoka kwa watu wengine ambao hauishi nao pia husaidia kuzuia kuenea kwa COVID-19.

Uchunguzi unaonyesha kuwa chanjo hizi ni bora zaidi kwa kuzuia COVID-19. Wataalamu pia wanasema kuwa chanjo hizi za COVID-19 zitasaidia kuzuia kuwa mgonjwa zaidi hata ukiambukizwa. Chanjo hizi haziwezi kukupa ugonjwa wenyewe.

